وَقَفَاتٌ مُخْتَصَرَةٌ فِي بَيَانِ

حُقُوقِ الأُخُوَّةِ

VIDOKEZO VIFUPI KATIKA KUBAINISHA

HAKI ZA UDUGU

Mtunzi

Sheikh. D. Muhammad Bin Ghalib Al-'Umari

Mfasiri

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila sifa njema anastahiki Mola wa walimwengu wote, na swala na salamu zimuendee Mtume wetu Muhammadﷺ, Jamaa zake na Maswahaba wake.

Baada ya haya: Hivi ni Vidokezo vichache katika kubainisha **Haki za Udugu kwa ajili ya Allaah**, nimependelea kuzikusanya kutoka kwenye dalili za Qur'an Sunnah na maneno ya Salaf; kwa sababu ya uzembe mkubwa unaoonekana, ambao ni kuacha kuitunza haki hii iliyo kubwa, na urahisi wa kutengana baina ya ndugu bila sababu halali za kisheria, wala kuchunga misingi ya Dini; lakini kwa sababu tu ya kutoafikiana kitabia au katika matamanio ya nafsi na tamaa[(1)]. Kwa hiyo ninasema kwa kufupisha maneno ili itimie kwa hilo kufikia kwenye lile nililokusudia.

1- **Ninasema (Abu Halima):** Alhamdulillaahi, baada ya kukipata na kusoma kipeperushi hiki na kunufaika na yale yaliyokusanywa ndani yake pamoja na uchache wa kurasa zake, nikaona niandike katika lugha ya Kiswahili ili yaenee manufaa yake kwa watu wengi katika jamii yetu na kila anaeweza kusoma lugha hii ya Kiswahili. Ni kweli haki nyingi za Udugu wa Kiislamu zimepotea hasa katika zama zetu, watu hudai wanapendana kwa ajili Allaah au kwa ajili ya Dini, lakini katika muamala wao ni tafauti na madai hayo! Utampata mtu anamchukia ndugu yake Muislamu mpaka kufikia kumtenga, kwa sababu tu ya maslahi fulani ya kidunia aliyotarajia kutoka kwake kisha ameyakosa n.k. bali mpaka kwa wenye kusoma Dini na kuilingania; wapo waliovunja Udugu wao uliojengwa na Itikadi sahihi ya Ahlus Sunnah, wala si Mali, Ukabila n.k. wameipoteza neema hii kubwa kwa duni thamani, Allaah anawakumbusha Maswahaba kuhusu neema ya Udugu wao:

﴿وَٱذۡكُرُواْ نِعۡمَتَ ٱللَّهِ عَلَيۡكُمۡ إِذۡ كُنتُمۡ أَعۡدَآءٗ فَأَلَّفَ بَيۡنَ قُلُوبِكُمۡ فَأَصۡبَحۡتُم بِنِعۡمَتِهِۦٓ إِخۡوَٰنٗا﴾

"Na kumbukeni neema ya Allaah iliyo juu yenu, pindi mlipokuwa nyinyi kwa nyinyi ni maadui, naye akaziunganisha nyoyo zenu, kwa neema yake mkawa ndugu" **Surat Aal Imraan/103.**

Je, wangapi miongoni mwetu wameunganishwa na Manhaji hii ya Salaf, na wengine hawakuwahi kujuana hapo kabla!, mpaka umefika muungano wetu huu (kwa taufiq ya Allaah) mtu anatembea Nchi nzima bila wasiwasi kuwa atampata huko ndugu anaejinasibisha na Manhaj hii ya haki!. Je haitoshi kwa hili kusamehe, kusahau na kuzika tafauti zetu?! Je haijafika mahali ukamsamehe ndugu yako aliyekukosea wewe binafsi muda wa kuwa mmeunganishwa na Dini na Sunnah?! Amesema Ibn Kathiir **-Allaah amrehemu-** wakati anaielezea Aya ya **(67) ya Surat Az-Zukhruf**: **[Kila urafiki (uliojengwa) kwa ajili ya asiyekuwa Allaah, siku ya kiama utageuka kuwa ni Uadui, ila Udugu uliokuwa kwa ajili ya Allaah, huo ni wenye kudumu muda mrefu].** Ndugu yangu muislamu, (Sunni, Salafy) tambua tuna dhima kubwa ya kudumisha Udugu na Urafiki wetu huu kwa ajili ya Allaah. **tunamuomba Allaah audumishe udugu wetu na authibitishe mpaka siku ya kukutana nae.**

Kidokezo cha Kwanza:
Mtu kupupia (rafiki) mwenye Dini

Amesema Mtume ﷺ

«الرَّجُلُ عَلَى دِينِ خَلِيلِهِ، فَلْيَنْظُرْ أَحَدُكُمْ مَنْ يُخَالِلُ»

"Mtu yupo juu ya dini ya ndugu yake, basi na atazame mmoja wenu ni nani atamfanya kuwa rafiki"[2].

Pia amesema:

«مَثَلُ الجَلِيسِ الصَّالِحِ وَالسَّوْءِ، كَحَامِلِ المِسْكِ وَنَافِخِ الكِيرِ، فَحَامِلُ المِسْكِ: إِمَّا أَنْ يُحْذِيَكَ، وَإِمَّا أَنْ تَبْتَاعَ مِنْهُ، وَإِمَّا أَنْ تَجِدَ مِنْهُ رِيحًا طَيِّبَةً، وَنَافِخُ الكِيرِ: إِمَّا أَنْ يُحْرِقَ ثِيَابَكَ، وَإِمَّا أَنْ تَجِدَ رِيحًا خَبِيثَةً»

"Mfano wa rafiki mwema na rafiki muovu ni sawa na muuza uturi/manukato na mfua vyuma. Muuza uturi: ima atakupatia (bure) au utanunua au utapata kutoka kwake harufu nzuri. Na mfua vyuma: ataunguza nguo yako, au utapata harufu mbaya"[3].

Na imepokewa kwamba Bilal Bin Saad **-Allaah amrehemu-** alikuwa anasema:

«أَخٌ لَكَ كُلَّمَا لَقِيكَ ذَكَّرَكَ بِحَظِّكَ مِنَ اللهِ خَيْرٌ لَكَ مِنْ أَخٍ كُلَّمَا لَقِيَكَ وَضَعَ فِي كَفِّكَ دِينَارًا»

"Ndugu yako (ambaye) kila anapokukuta anakukumbusha nafasi yako kwa Allaah, ni bora kuliko yule ambaye kila anapokukuta anaweka katika mkono wako wako Dinari (anakupa pesa"[4].

Na amesema Malik Bin Diinar kumwambia Mughira Bin Habib رَحِمَهُمَا اللهُ :

«يَا مُغِيرَةُ كُلُّ أَخٍ وَجَلِيسٍ وَصَاحِبٍ لَا تَسْتَفِيدُ مِنْهُ فِي دِينِكَ خَيْرًا فَانْبِذْ عَنْكَ صُحْبَتَهُ»

"Ewe Mughira, rafiki yeyote au swahiba ambaye haunufaiki nae katika dini yako kwa (kupata) kheri, basi utupilie mbali usuhuba wake huo"[5].

2- Sunan Tirmidh [2378].
3- Bukhari (5534) na Muslim [146].
4- Hilyatul Auliyaa [Jz. 5, Uk. 225].
5- Hilytaul Auliyaa [Jz. 6, Uk. 248].

Kidokezo cha Pili:
Kuvumiliana baina ya ndugu

Allaah Subhaanahu wata'alaa wakati anaelezea sifa za watu wenye taqwa ambao Alaah amewaandalia pepo, akasema:

﴿وَٱلۡكَٰظِمِينَ ٱلۡغَيۡظَ وَٱلۡعَافِينَ عَنِ ٱلنَّاسِۗ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلۡمُحۡسِنِينَ﴾

"Na wenye kuzuia ghadhabu (hasira), na wasamehevu kwa watu, na Allaah huwapenda wenye kufanya wema"[6].

Na Mtume ﷺ amesema:

«وَمَا زَادَ اللهُ عَبْدًا بِعَفْوٍ، إِلَّا عِزًّا، وَمَا تَوَاضَعَ أَحَدٌ لِلَّهِ إِلَّا رَفَعَهُ اللهُ»

"Na Allaah hajamzidishia mja yeyote kwa sababu ya kusamehe isipokuwa (humpa ziada ya) utukufu, na hakuna yeyote anaenyenyekea kwa ajili ya Allaah isipokuwa Allaah humwinua"[7].

Na imepokewa ya kwamba Ibn Sammaak **-Allaah amrehemu-** aligombana na rafiki yake, yule rafiki yake akasema:

"المِيْعَادُ غَدًا نَتَعَاقَبُ"

"Ahadi (yetu) ya kugombana ni kesho",

Yeye akamjibu akasema:

"بَل المِيْعَادُ غَدًا نَتَغَافَرُ"

"Bali kesho ndio ahadi yetu ya kusameheana"[8].

6- Surat Aal Imraan/134.
7- Muslim (69).
8- Shu'abul iimaan (Jz. 1, Uk. 324).

Kidokezo cha Tatu:
Kudhihirisha upendo kwa kuusimulia na kwa vitendo

Amesema Mtume wetu ﷺ:

«إِذَا أَحَبَّ الرَّجُلُ الرَّجُلَ فَلْيُخْبِرْهُ أَنَّهُ أَحَبَّهُ»

"Mtu akimpenda mtu mwingine, basi amueleze kwamba yeye anampenda"[9].

Na imepokewa kutoka kwa Sufian Bin 'uyaina **-Allaah amrehemu-** kwamba amesema:

«سَمِعْتُ مُسَاوِرًا الْوَرَّاقَ يَحْلِفُ بِاللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ مَا كُنْتُ أَقُولُ لِرَجُلٍ: «إِنِّي أُحِبُّكَ فِي اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ فَأَمْنَعُهُ شَيْئًا مِنَ الدُّنْيَا»

"Nilimskia Musaawir Al-Warraaq akimuapia kwa Allaah 'Azza Wajalla, (akisema): Sikuwa mimi nikimwambia mtu: "Nakupenda kwa ajili ya Allaah 'Azza Wajalla kisha namzuilia yeye jambo la kilimwengu"[10].

Maana yake: Mtu yeyote ambaye yeye aliwahi kumwambia kwamba anampenda kwa ajili ya Allaah, basi hawezi kumnyima kitu chochote katika vitu kidunia; hii ni ishara kwamba udugu uliojengwa juu ya msingi wa Dini una thamani zaidi kuliko thamani ya mali, cheo n.k. Tunamuomba Allaah atujaalie tupendane kwa ajili yake kwa ajili ya kutaraji pepo yake.

Amesema Ibn Taymiyyah**-Allaah amrehemu-**:

وَالْمُحِبُّ لِلَّهِ إذَا أَحَبّ شَخْصًا لِلَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ مَحْبُوبُهُ فَهُوَ يُحِبُّ أَنْ يَجْذِبَهُ إلَى اللَّهِ تَعَالَى وَكُلٌّ مِنْ الْمُحِبِّ لِلَّهِ وَالْمَحْبُوبِ لِلَّهِ يُجْذَبُ إلَى اللَّهِ

"Mwenye kupenda kwa ajili ya Allaah, anapompenda mtu basi Allaah na yeye humpemda, na anapenda kumvuta (rafiki yake) kumuelekeza kwa Allaah Ta'alaa, na kila mmoja katika yule Mwenye kupenda na Mwenye kupendwa huwa anavutwa kuelekea kwa Allaah"[11].

---

[9]- Kitabu: [Adabul Mufrad] (279). Cha Imam Bukhari.
[10]- Kitabu: [Al-Ikhwaan] (202). Cha Ibn Abi Ddun-ya.
[11]- Kitabu: [Majmuul Fataawa] (Jz. 10, Uk. 608). Fataawa za Ibn Taymiyyah.

Kidokezo cha Nne:
Kupeana nasaha baina ya ndugu

Amesema Mtume ﷺ:

«الدِّينُ النَّصِيحَةُ» قُلْنَا: لِمَنْ؟ قَالَ: «لِلَّهِ وَلِكِتَابِهِ وَلِرَسُولِهِ وَلِأَئِمَّةِ الْمُسْلِمِينَ وَعَامَّتِهِمْ»

"Dini ni kunasihiana". Tukasema sisi: nasaha hizo ni kwanani? Akasema: "Kwa ajili ya Allaah na Mtume wake na viongozi wa waislamu na watu wao"[12].

Na Hasan Al-Basri **-Allaah amrehemu-** alikuwa akisema:

«إِخْوَانُنَا أَحَبُّ إِلَيْنَا مِنْ أَهْلِنَا وَأَوْلَادِنَا لِأَنَّ أَهْلَنَا يُذَكِّرُوْنَنَا بِالدُّنْيَا وَإِخْوَانُنَا يُذَكِّرُوْنَنَا بِالْآخِرَةِ»

"Ndugu zetu wanapendeza zaidi kwetu kuliko wake zetu na watoto wetu, kwa sababu wake zetu wanatukumbusha sisi dunia, na ndugu zetu wanatukumbusha sisi akhera"[13].

Kidokezo cha Tano:
Kupendeleana (kheri) baina ya marafiki

Allaah Ta'alaa amewasifu Maswahaba wa Mtume wake ﷺ akasema:

﴿وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِۦ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ﴾

"Na wanawapendelea (ndugu zao) kuliko nafsi zao ijapokuwa upo kwao uhitaji. Na yeyote atakaekingwa na ubakhili wa nafsi yake basi hao ndio wenye kufaulu"[14].

Amesema Abbas Bin Dihqaan **-Allaah amrehemu-:**

«مَا خَرَجَ أَحَدٌ مِن الدُّنْيَا كَمَا دَخَلَهَا إِلَّا بِشْرُبْنُ الحَرْثِ فَإِنَّهُ أَتَاهُ رَجُلٌ فِي مَرَضِهِ فَشَكَا إِلَيْهِ الحَاجَةَ فَنَزَعَ قَمِيْصَهُ وَأَعْطَاهُ إِيَّاهُ وَاسْتَعَارَ ثَوْبُاً فَمَاتَ فِيْهِ»

"Hakuna yeyote aliyeondoka duniani kama alivyokuja, isipokuwa Bishru Bin Harthi, kwa sababu wakati wa maradhi yake alimjia yeye mtu mmoja akamshatakia yeye shida yake; basi (Bishru) akavua kanzu yake akampatia, kisha akaazima nguo na akafa nayo"[15].

12- Muslim (95).
13- Kitabu: [Ihyaau Uluumi Ddiin] (Jz.2, Uk. 176)
14- Surat Al-Hashri/9.
15- Kitabu: [Ihyaau Uluumi Ddiin] (Jz. 3, Uk. 258).

Kidokezo cha Sita:
Kupuuza na Kusahau (yaliyopita)

Amesema Allaah Ta'alaa:

﴿وَإِذْ أَسَرَّ ٱلنَّبِيُّ إِلَىٰ بَعْضِ أَزْوَٰجِهِۦ حَدِيثًا فَلَمَّا نَبَّأَتْ بِهِۦ وَأَظْهَرَهُ ٱللَّهُ عَلَيْهِ عَرَّفَ بَعْضَهُۥ وَأَعْرَضَ عَنۢ بَعْضٍ ۖ فَلَمَّا نَبَّأَهَا بِهِۦ قَالَتْ مَنْ أَنۢبَأَكَ هَٰذَا ۖ قَالَ نَبَّأَنِىَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْخَبِيرُ﴾

"Kumbuka pale alipofanya siri khabari Mtume ﷺ kwa wakeze, basi pindi (Hafsa) alipomueleza (Aisha) na Allaah alimueleza Mtume wake juu ya hilo, Mtume ﷺ alielezea baadhi na akanyamazia baadhi nyingine. Wakati Mtume ﷺ alipomwambia (Hafsa): Kwanini habari ile umemwambia (Aisha)? Akasema: Ni nani aliyekueleza haya? Akasema (Mtume ﷺ): Amenieleza mimi Allaah aliye Mjuzi Mwenye kujua habari (zote)". Tahriim/3.

Amesema Imam Qurtubi **-Allaah amrehemu-:**

«وَأَعْرَضَ عَنْ بَعْضٍ تَكَرُّمًا، قَالَهُ السُّدِّيُّ. وَقَالَ الْحَسَنُ: مَا اسْتَقْصَى كَرِيمٌ قَطُّ»

Amesema As-Suddi: "Na akanyamazia baadhi nyingine kwa ajili ya kupuuza". Na amesema A-Hasan: "Hakuwahi mtu mkarimu kudadisi". Tafsirul Qurtubi (Jz. 18, Uk. 187).

Kidokezo cha Saba:
Kuufurahia Udugu huu (wa Dini)

Amesema Mtume ﷺ:

ثَلاَثٌ مَنْ كُنَّ فِيهِ وَجَدَ حَلاَوَةَ الإِيمَانِ...، وَأَنْ يُحِبَّ المَرْءَ لاَ يُحِبُّهُ إِلَّا لِلَّهِ

"Mambo matatu yule ambaye yatakusanyika kwake, atapata ladha ya Imani... (miongoni mwa hayo), na awe anampende mtu, hampendi isipikuwa kwa ajili ya Allaah". Bukhari (16).

Amesema Umar Ibnul Khatwaab **-Allaah amuwie radhi-**:

«إِذَا رَزَقَكُمُ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ مَوَدَّةَ امْرِئٍ مُسْلِمٍ فَتَشَبَّثُوا بِهَا»

"Ikiwa Allaah 'Azza Wajalla amewaruzukuni mapenzi ya mtu Muislamu, basi shikamana nayo (mapenzi hayo)". [Al-Ikhwaan] (Uk. 81). Cha Ibn Abi Ddun-ya.

Kidokezo cha Nane:
Kutembeleana na Kutafutana

Imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ:

«أَنَّ رَجُلًا زَارَ أَخًا لَهُ فِي قَرْيَةٍ أُخْرَى، فَأَرْصَدَ اللهُ لَهُ عَلَى مَدْرَجَتِهِ مَلَكًا، فَلَمَّا أَتَى عَلَيْهِ، قَالَ: أَيْنَ تُرِيدُ؟ قَالَ: أُرِيدُ أَخًا لِي فِي هَذِهِ الْقَرْيَةِ، قَالَ: هَلْ لَكَ عَلَيْهِ مِنْ نِعْمَةٍ تَرُبُّهَا؟ قَالَ: لَا، غَيْرَ أَنِّي أَحْبَبْتُهُ فِي اللهِ عَزَّ وَجَلَّ، قَالَ: فَإِنِّي رَسُولُ اللهِ إِلَيْكَ، بِأَنَّ اللهَ قَدْ أَحَبَّكَ كَمَا أَحْبَبْتَهُ فِيهِ»

"Kwamba mtu mmoja alimtembelea ndugu yake katika mji mwingine, Allaah akamuwekea yeye katika njia yake malaika anaemngojea, wakati alimpofikia (yule malaika) akamuuliza: unakusudia kwenda wapi? Akajibu: namkusudia ndugu yangu (anaishi) katika mji huu. Akamuuliza: Je kuna neema yoyote kwake unayotarajia kuipata? Akajibu: hapana, isipokuwa mimi nimempenda yeye kwa ajili ya Allaah 'Azza Wajalla. Akasema (yule malaika): mimi ni mjumbe wa Allaah kwako (nimetumwa nikwambie): kwamba Allaah amekupenda kama ulivyompenda huyo (rafiki yako) kwa ajili yake"[16].

Na Imam Nnawawi **-Allaah amrehemu-** wakati alipotaja faida zinazopatikana katika hadithi hii, akasema:

«فِي هَذَا الْحَدِيثِ فَضْلُ الْمَحَبَّةِ فِي اللَّهِ تَعَالَى وَأَنَّهَا سَبَبٌ لِحُبِّ اللَّهِ تَعَالَى الْعَبْدَ وَفِيهِ فَضِيلَةُ زِيَارَةِ الصَّالِحِينَ وَالْأَصْحَابِ»

"Kuna katika hadithi hii fadhila za kupendana kwa ajili ya Allaah Ta'alaa, na kwamba (mapenzi) hayo ni sababu ya Allaah kumpenda mja wake, na kuna ndani yake fadhila za kuwatembelea watu na marafiki walio wema"[17].

Na alikuwa Omar Ibnil Khatwaab **-Allaah amuwie radhi-** anamkumbuka mtu katika ndugu zake wakati wa usiku, halafu anasema:

«يَا طُولَهَا مِنْ لَيْلَةٍ». فَإِذَا صَلَّى الْمَكْتُوبَةَ غَدَا إِلَيْهِ فَإِذَا الْتَقَيَا عَانَقَهُ.

"Eeh, si urefu ulioje wa usiku", na akimaliza kuswali swala ya asubuhi anarauka kumfuata, na pindi wakikutana anamkumbatia[18].

16- Muslim (38).
17- Sharhi Muslim (Jz. 16, Uk. 124).
18- Kitabu: [Al-Ikhwaan] (Uk. 70). Cha Ibn Abi Ddun-ya

Kidokezo cha Tisa:
Kusaidiana katika wema

Amesema Allaah Ta’alaa:

﴿وَتَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡبِرِّ وَٱلتَّقۡوَىٰۖ﴾

“Na saidianeni katika wema na taqwa”[19].

Na Mtume ﷺ amesema:

«لاَ يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ، حَتَّى يُحِبَّ لِأَخِيهِ مَا يُحِبُّ لِنَفْسِهِ»

“Haitatimia Imani ya mmoja wenu mpaka apende apate ndugu yake ambalo anapenda ipate nafsi yake”[20].

Na aliulizwa imam Sufian Bin ‘Uyaina **-Allaah amrehemu-,** kuhusiana na kauli ya Allaah:

﴿وَتَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡبِرِّ وَٱلتَّقۡوَىٰۖ﴾

“Na saidianeni katika wema na taqwa”.

Akasema:

«هُوَ أَنْ تَعْمَلَ بِهِ، وَتَدْعُوَ إِلَيْهِ، وَتُعِيْنَ فِيْهِ، وَتَدُلَّ عَلَيْهِ»

“Ni kuutenda huo wema, kuulingania, kusaidia ndani yake, na kuuonyesha”.

19- Surat Al-Maaida/2.

20- Bukhari (13) na Muslim (71).

Kidokezo cha Kumi:
Kuvumilia juu ya mapungufu ya wengine, katika isiyokuwa jambo la Dini

Subra ni yenye kuhitajika katika hali zake zote tatu.

Amesema Allaah wakati akiwasifia waumini:

﴿وَتَوَاصَوْاْ بِٱلْحَقِّ وَتَوَاصَوْاْ بِٱلصَّبْرِ﴾

"Na wakausiana kushikamana na haki na wakausiana kusubiri"[21].

Amesema Yahya Bin Muadh **-Allaah amrehemu-**:

حَقِيقَةُ الْمَحَبَّةِ: أَنَّهَا لَا تَزِيدُ بِالْبِرِّ، وَلَا تَنْقُصُ بِالْجَفَاءِ

"Mapenzi ya kweli (kwa ajili ya Allaah): hayazidi kwa wema wala hayapungui kwa kuchukizwa"[22].

Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah

Jumamosi 9/5/1444H – 3/12/2022M.

Pongwe Tanga

Tanzania.

Simu: +255 715 263 253

21- Surat Al-'Asri/3.

22- Kitabu: [Az-Zuhdu war-Raqaaiq] (Uk. 67). Cha Al-Khatibu Al-Baghdaadi.